



**MAISHA  
MAPYA  
NDANI  
YA KRISTO**

**Toleo la 3**

---

**Kuishi pamoja sisi kwa sisi**

Hili ni chapisho la kwanza la Maisha Mapya ndani ya Kristo Toleo la 3. Kusudi lake ni kusaidia kutoa msingi imara kwa maisha yako ya Kikristo, hasa hasa katika eneo la mahusiano na waamini wengine.

Kwa maelezo zaidi tuandikie barua pepe: [info@nuevavidaencristo.org](mailto:info@nuevavidaencristo.org)

Unaweza pia kupata nakala ya kitabu hiki na vitabu vingine kuititia mtandao huu:  
**[www.NewLifeDiscipleship.com](http://www.NewLifeDiscipleship.com)**

Matoleo yote yanapatikana pia katika Kiswahili, Kiengereza, Kifaransa, Kispaniola, Kireno. Matoleo mengine yanapatikana katika lugha zingine kama Kinyarwanda.

Toleo hili linapatikana pia katika mfumo wa PDF ambao unahitaji Adobe Reader (zamani ulijulikana kama Adobe Acrobat).

Umeruhusiwa kufanya nakala ya nyenzo hii kwa masharti kwamba unaelezea chanzo ya awali na kutofanya mabadiliko au nyongeza kwa maudhui yake.

Toleo la Kwanza 2005. © Mark Robinson  
First Editionin Kiswahili 2015

Kimetengenezwa na Mark Robinson  
Camino Global  
8625 La Prada Dr., Dallas, TX 75228, USA  
Kimetafsiriwa na Sammy Awami

# **YALIYOMO**

Mwongozo wa Mwalimu .....	4
Hatua ya 1 “Sisi kwa Sisi” .....	6
Hatua ya 2 Pendareni ninyi kwa ninyi .....	8
Hatua ya 3 Zaidi juu ya kupendana .....	10
Hatua ya 4 Tianeni moyo .....	12
Hatua ya 5 Hudumianeni ninyi kwa ninyi .....	14
Hatua ya 6 Vumilianeni .....	16
Hatua ya 7 Sameheaneni .....	18
Hatua ya 8 Pokeaneni .....	20
Hatua ya 9 Inuaneni .....	22
Hatua ya 10 Peaneni maonyo .....	24
Hatua ya 11 Salimianeni Muwe wakarimu kwenu ninyi kwa ninyi .....	26
Nyongeza .....	28

# MUONGOZO WA MWALIMU



1. Tunakupongeza kwa kupokea changamoto ya kuwaongoza waumini wapya kwa kutumia Maisha Mapya ndani ya Kristo kama muongozo wako. Matokeo ya mafundisho haya yanaweza kusababisha matunda ya milele.
2. Ifanye Biblia kuwa mamlaka yako katika kujibu maswali. Wanafunzi wanapaswa kuangalia vifungu vya Biblia wenyewe na wajaribu kujibu maswali kulingana na kile Biblia inachosema.

Baadhi ya waamini wapya wanahitaji msaada kwa ufupi juu ya kutafuta mistari mbalimbali katika Biblia zao.
3. Mwongozo huu unaweza kutumika katika namna mbalimbali. Mara nyingi, utajifunza somo moja kwa wiki, na kuwatia moyo wanafunzi kufanya mazoezi yote katika kila somo.
4. Jitahidi usifanye vipindi vyako vikawa virefu sana. Hakikisha unawaangalia wanafunzi wako kuona kama bado wanakufta/wanakusikiliza.
5. Watie moyo wanafunzi kujibu maswali kwa maneno yao wenyewe. Wajitahidi kukwepa kuna kili Biblia neno kwa neno. Kutumia maneno yao wenyewe, kutawasaidia kuchambua vizuri maana ya maneno waliyoyasoma
6. Epuka kuhubiri. Tumia maswali kugundua wanafunzi wanaelewa nini na kuamsha ushiriki mzuri darasani.
7. Wewe mwenyewe ujiandae vizuri kwa kila somo. Ukiwa kama mwalimu, unapaswa kufahamu unachokwenda kufundisha na mantiki za msingi za kila somo.

Maandalizi yako yajumuushe maombi kwa wanafunzi wako na kwa moyo wako mwenyewe kuijandaa kwa ajili ya somo

8. Jaribu kuwafanya wanafunzi kufikiria juu ya namna ya kulitumia somo kwa maisha yao ya kila siku. Wasaidie kuelewa matumizi ya kila siku ya somo



Kila somo lina vipengele vyenye alama iliyoandikwa SIMAMA. Hizi zimebekwa kwa ajili ya wanafunzi kusimama na kufikiria juu ya matumizi ya somo katika maisha yao ya kila siku. Chukua muda kutafakari juu ya vipengele hivi.

Mazoezi katika viboksi pembedi mwa kila somo yametengenezwa kwa sababu hiyo. Yatumie.

9. Wasaidie wanafunzi wajenge tabia ya maombi. Wafundishe kwa kuomba nao.
10. Ni muhimu ukaelewa kwamba ufuasi ni zaidi ya kusoma masomo katika Maisha Mapya ndani ya Kristo. Ufuasi maana yake ni mabadiriko ya maisha kwa mfuasi.

Muongozo huu ni msaada wa mwanzo tu. Wanafunzi wanahitaji msaada endelevu katika kutafuta mabadiriko ya tabia zao, namna wainavyofikiri, nk.

11. Ni muhimu sana kwamba wafuasi wajifunze tabia kama vile kusoma Biblia kila siku, kuomba na kukariri mistari ya Biblia.


Mwanzoni mwa kila somo, tenga muda kujikumbusha mstari waliokariri wakati uliopita na wauzile wanaendeleaje katika kusoma Biblia kila siku. Usiwakaripie wanafunzi ambao hawajamaliza baadhi ya mazoezi uliyowapa, lakini hakikisha unawatia moyo kuyamaliza

12. Uwe makini kwa kile ambacho Mungu anakifanya katika maisha ya mfuasi. Chukua muda katika kila somo kujibu swali lolote lile wanaloeweza kuwa nalo, au kuwasaidia katika matatizo wanayokumbana nayo katika maisha yao binafsi.

Kumbuka pia kwamba kuna wakati haitakua rahisi upitia kila swali katika somo kwasababu ya ufupi wa muda. Katika hali kama hizi, chagua maswali yaliyo na umuhimu mkubwa ambayo mnaweza kuyajadili.



**“Na kama  
mnavyotaka watu  
wawatendee ninyi,  
watendeeni vivyo  
hivyo.” Luka 6:31**



## Hatua ya 1 “Sisi kwa Sisi”

### KWELI AMA SI KWELI

Tunapaswa kuwatendea wengine vile wao wanavyotutendea.  
Ili mradi simuumizi mtu, basi nafanya kile ambacho Mungu  
anantaka nifanye.  
Wakristo wameitwa kuwasaidia ndugu zao katika Kristo.

### KUFANYAKAZI KWA PAMOJA

Mmisionari mmoja hapa Afrika aliwaona wakoma wawili wakipanda mbegu shambani. Mmoja wao hakuwa na mikono yote miwili kwasababu ililiwa na ukoma. Yule mwininge hakuwa na miguu naye kwasababu ya ugonjwa huo mbaya kabisa. Yule mkoma asiyekuwa na mikono alimbeba mabegani yule mwenzake asiyekuwa na miguu. Yule aliyejkuwa na mikono alibeba mfuko wa mbegu ambaao alidondosha mbegu ardhini, wakati ambapo yule mkoma mwininge alitumia miguu yake kushindilia zile mbegu aridhini.

Kwa pamoja waliweza kufanya kazi ya mtu mmoja mwenye afya.<sup>1</sup>

Tunapokuja kwa Kristo, tunafanyika sehemu ya Kanisa lake, tukiwa na kaka na dada katika Kristo duniani kote. Kanisa ni familia yetu mpya, kimbilio letu na kusanyiko letu la msaada. Lakini kama ilivyo katika familia nyinezo, nyakati zingine inakuwa vigumu kupatana na kila mtu kwasababu sisi sote tunatofautiana sana. Tunawezaje kuishi pamoja kwa umoja? Hebu tuangalie baadhi ya kanuni ambazo Mungu ametupa ambazo zinazoweza kutusidia kuishi kwa amani kati yetu sisi kwa sisi

### KANUNI KUU

1. Luka 6:31 ina kanuni tunayoiita “kanuni kuu”. Hebu andika kwa ufupi na kwa maneno yako kanuni hiyo inasemaje.
- 
- 



2. Hebu tuangalie maana halisi ya kanuni kuu katika vifungu viuatavyo:

Luka 6:27 \_\_\_\_\_ zenu \_\_\_\_\_ na watendeeni \_\_\_\_\_

wale ambaao \_\_\_\_\_.

Luka 6: 28 \_\_\_\_\_ wale ambaao \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_

wale ambaao \_\_\_\_\_.

Kutii amri hii ya Kristo ni zaidi ya kuwaumiza wengine, ina maana kuwatendea wengine vizuri, kama vile ambavyo wewe ungependa kutendewa. Hatupaswi kuwaumiza wengine; lakini kanuni kuu inakwenda hatua moja mbele zaidi, inatusihi kuwatendea wengine kwa upendo na rehema, hata kama wanatutendea sisi kwa ubaya.



*Alama hii inakuashiria USIMAME kwa muda mfupi. Chukua muda kutafakari juu ya yafuatayo:*

*Ungependa wengine wakutendeaje? Je hivyo ndivyo unavyowatendea wao?*

*Fikiri juu ya wakati ule wiki hii ulivyojiskia vibaya jinsi ulivyomtendea yule mtu.*

*Ungeweza kufanyaje ili kumtendea vyema?*

### TUNAPASWA KUTENDEAJE SISI KWA SISI?

“Sisi kwa Sisi”: Kuna vifungu vingi sana katika maandiko vinavyotumia hii sentensi “sisi kwa sisi.” Kila kifungu kinatusaidia kufafanua jinsi gani tunaweza kuitii kanuni kuu na hivyo kuishi kwa amani “sisi kwa sisi” Andika amri moja au zaidi ya moja zinazotajwa katika kila vifungu vifuatavyo:

## FIKIRI JUU YA HILI

Siku moja John F. Kennedy alivahi kusema: "...usiulize nchi yako itaku-fanyia nini; uliza utaifanyia nini nchi yako."

Hebu fikiria kitakachotokea katika maisha yako ikiwa ungesema, "usiulize Wakristo wengine wanatakfanyia nini; uliza unawenza kuwfanyia nini."



## KUWAHUDUMIA WENGINE

Una karama/vipaji gani ambavyo vinawenza kukusaidia kuwatukia wengine? Muulize mchungaji wako au Mkristo aliyekomaa apendekeze namna unayoweza kutumika katika kanisa lako.

3. Marko 9:50 \_\_\_\_\_
4. Yohana 13:34 \_\_\_\_\_
5. Warumi 14:13 \_\_\_\_\_  
badala ya \_\_\_\_\_
6. Warumi 12:15 \_\_\_\_\_  
na \_\_\_\_\_
7. Warumi 15:1 \_\_\_\_\_
8. Warumi 15:2 \_\_\_\_\_
9. Warumi 15:7 \_\_\_\_\_
10. Warumi 15:14 \_\_\_\_\_
11. Warumi 16:16 \_\_\_\_\_
12. Wagalatia 5:13 \_\_\_\_\_
13. Wagalatia 5:26 \_\_\_\_\_
14. Wagalatia 6:2 \_\_\_\_\_
15. Waefeso 4:2 \_\_\_\_\_
16. Wakolosai 3:13 \_\_\_\_\_
17. Wakolosai 3:16 \_\_\_\_\_
18. 1 Wathesalonike 4:18 \_\_\_\_\_
19. 1 Wathesalonike 5:11 \_\_\_\_\_ & \_\_\_\_\_
20. Waebrania 10:24-25 \_\_\_\_\_  
& \_\_\_\_\_
21. Yakobo 5:16 \_\_\_\_\_ & \_\_\_\_\_
22. 1 Petro 4:9 \_\_\_\_\_



Hadi hivi sasa, umeishije kama Mkristo? Je umekua unajali zaidi juu ya ukuaji wako au umewasaidia wengine pia kukua?

## KUWA IMARA



**Soma Wagalatia 1-6 na Tito**  
wiki hii (kila sura kwa siku).

**Kariri Luka 6:31.**

"Na kama mnavyotaka watu wawatendee ninyi, waten-deeni vivyo hivyo"

Katika mzani wa moja hadi kumi—kumi ikiwa ni bora zaidi – jipime ni kwa kiasi gani umekua ukiifuata "sisi kwa sisi" 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10

Chagua moja ya tabia zinazotajwa katika somo hili ambazo unawenza kuzitilia mkazo wiki hii. zipi? \_\_\_\_\_

Unawezaje kuitumia tabia hii wiki hii kukusaidia kuwa karibu zaidi na waamini wengine? Taja kinagaubaga. \_\_\_\_\_

## Hatua ya 2

# Mpendane Ninyi kwa Ninyi



### KWELI AMA SI KWELI

- \_\_\_\_\_ Kuwapenda Wakristo wengine kutauonesha ulimwengu kwamba sisi ni watoto wa Mungu kweli kweli.
- \_\_\_\_\_ Unaweza kumpenda Mungu na kumchukia mtu kwa wakati mmoja.
- \_\_\_\_\_ Upendo wa kweli unaonekana kwa matendo yetu, na si kwa maneno yetu tu

### KUWAPENDA KAKA NA DADA ZANGU

Wakati tunapaswa kuwapenda watu wote, tunatakiwa kuwapenda hasa kaka na dada zetu katika Kristo (1 Petro 2:17). Kama familia, tunao wajibu wa kujaliana na kusaidiana sisi kwa sisi. Kanisa letu linapaswa kuwa kimbilio na mahali ambapo tunapata umoja na upendo ambao umekua haba sana siku hizi ulimwenguni.

1. Kwanini kuwapenda waamini wengine ni muhimu sana? Yohana 13:34-35

mst. 34 \_\_\_\_\_


mst. 35 \_\_\_\_\_

Kuwapenda waamini wengine sio amri tu, ni kama vazi la sare linalotutambulisha sisi kama wafuasi wa Kristo, na kututofautisha na wale wasiomfahamu.

- 2 Nani mfano wetu katika swala la upendo? mst. 34 \_\_\_\_\_.



Warumi 5:6-8 inasema kwamba Mungu anatupenda, si kwasababu tunastahili, lakini kwasababu ya neema yake. Upendo ni asili yake (1 Yohana 4:8). Upendo wa Kristo hufikiri juu ya wengine, wakati upendo wa dunia ni wa kibinafsi, ukiuliza "Mimi nitafaidikaje hapa?" Fikiri juu ya upendo wako juu ya kaka na dada zako wa Kikristo. Unaweza kuitwa usio wa kibinafsi, au usio na masharti? Unafikiri zaidi kuhusu wengine au kuhusu wewe mwenyewe?



3. Upendo ni zaidi ya hisia nzuri kwa wengine; inahitaji vitendo. Ikiwa tunataka kupenda kama Kristo alivyopenda, tunahitaji kufanya nini? Yohana 15:10 \_\_\_\_\_

4. Upendo ni kipima joto chetu cha kiroho. Unamuonaje mtu anayejidai kuwa ni Mkristo mzuri wakati anamchukia ndugu yake? 1 Yohana 2:9-10 \_\_\_\_\_

5. I Yohana 3:18 Tusipende kwa \_\_\_\_\_ lakini kwa \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_  
Nini tofauti ya kupenda kwa maneno na kupenda kwa vitendo na kwa kweli? \_\_\_\_\_

Je kuna wakati unajifanya kuwapenda watu wakat I kiukweli hauwapendi? Maswali yafuatayo yataku-saidia kuelewa upendo wa kweli unahitaji nini hasa.

### UPENDO NA SADAKA

6. Kwa mujibu wa 1 Yohana 3:16, tunawezaje kuonyesha upendo wetu? \_\_\_\_\_

Je, ina maanisha kwamba tunapaswa kufa kweli kwa ajili ya wengine? \_\_\_\_\_

7. Ni mifano gani inayotolewa ya kuyatoa maisha yetu kwa ajili ya wengine? mst. 17 \_\_\_\_\_

Kuyapuuza mahitaji ya wengine inaonesha wazi kwamba hatuna upendo wa kutosha kama ambavyo tungependa kudhani.

## KUWA IMARA

**Soma Warumi 12,**  
**2 Yohana, 3 Yohana,**  
**2 Petro 1-3**  
(sura moja kwa siku).



## Kariri 1 Yohana 3:16

"*Katika hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu.*"

## FIKIRIA

Upendo ni zaidi ya hisia nzuri tu kwa wengine. Inahuisha tendo la makusudi. Mathayo 5:42-48 inatuambia kwamba Mungu huwaangazia jua waovo na walio wema. Tunatakiwa kuwapenda adui zetu na marafiki zetu pia. Hii inamaanisha kuwasamehe, kuwaombea, na kuwatendea vyema pale tunapotakiwa kuwafanya hivyo

Tengeneza mpango wa namna gani unaweza kupata na wale uliowakosea. Kumbuka kwamba usuruhi unahuisha kuomba msamaha na kusamehe pia.

Pitia tena yale masomo mawili yahusuyo msamaha katika Toleo la 2

*Andika mpango katika karatasi nyingine.*



Shinda uovo kwa wema  
Warumi 12:21

8. Toa mifano mingine ya namna gani unaweza kuyatoa maisha yako kwa ajili ya wengine. \_\_\_\_\_

9. Amri ya pili inasema: "mpende jirani yako kama nafsi yako." Mtu ali-pouliza: "Na jirani yangu ni nani," Yesu alijibu kwa Mfano wa Msamaria Mwema. Soma Luka 10:30-37..

Ni nani katika mfano huu alimpenda jirani yake kweli kweli? \_\_\_\_\_  
Unajuaje? \_\_\_\_\_

10. Hata kama kuhani na mlawi hawakuhusika na kupigwa kwa yule bwana, tunaweza kusema kwamba wao ni bora kuliko wale wanyang'anyi? Kwanini?

Ingawa tofauti hazionekani kuwa kubwa sana, kiukweli ni aina nyingine tu ya kuumiza kwasababu inaonesha kutokuwepo kwa upendo kwa wengine. Hata kama yule Msamaria hakuwa anatokea maeneo ya jirani, alimuonesha huruma mtu yule aliye kua ameumizwa. Alielewa kwamba "jirani" yake alikua ni ye yote yule mwenye shida ambaye Mungu alikua amemleta katika njia yake.

Pode-se resumir essa parábola assim:

- Wanyang'anyi: "Chochote kilichochako ni changu."
- Kuhani na Mlawi: "Chochote kilicho chetu ni chetu."
- Msamaria: "Chochote kilicho changu ni chetu."



*Fikiri jinsi unavyowatendea wengine. Andika ni mtazamo gani kati ya hii mitatu inayoelezea vizuri uhusiano wako na wa:*

Familia yako \_\_\_\_\_

Wafanyakazi au wanafunzi wenzako \_\_\_\_\_

Waumini wa kanisa lak \_\_\_\_\_

## INAKUWAJE IKIWA WAO HAWANITENDEI VYEMA?

*"Yeyote anaependekeza kufanya wema lazima asitegemee watu wamuondolee mawe katika njia yake, lakini lazima akubaliane na fungu lake kwa upole ikiwa wataweka hata mawe mengine juu"*<sup>2</sup>

11. Soma Warumi 12:17-21. Tunapaswa kuwarudishia vipi wale wasiotunden-dea vyema, kwa mujibu wa mistari ifuatayo?

mst. 17 \_\_\_\_\_

mst. 18 \_\_\_\_\_

mst. 19 \_\_\_\_\_

mst. 21 \_\_\_\_\_




*Tunaweza kuushinda uovu kwa wema. Kwa kiasi gani umefanikiwa katika kufanya hivyo?* \_\_\_\_\_

*Kama jibu lako ni "sio vizuri sana," ni nani ambaye hampatani vizuri?* \_\_\_\_\_

*Ni kitu gani kizuri unachoweza kufanya wiki hii kupunguza hali hiyo ya msuguano na mtu huyo?* \_\_\_\_\_

## Hatua ya 3

# Zaidi juu ya upendo



### KWELI AU SI KWELI

- \_\_\_\_\_ Badala ya kuulinda upendo, wivu utauharibu.
- \_\_\_\_\_ Upendo wa kweli hauangalii makosa ya wengine.
- \_\_\_\_\_ Haja ya kumiliki vitu inaweza kuharibu uwezo wangu wa kutengeneza mahusiano mazuri na wengine

### KUCHUKUA HATUA ZA UPENDO WA KWELI

1. Upendo ni nini? 1 Wakorintho 13:4-7 inaelezea upendo wa kweli, inaorodhesha tabia kumi na tano – saba zilizo nzuri na nane zisizo nzuri. Ziandike.

Upendo ni: \_\_\_\_\_

Upendo si: \_\_\_\_\_

2. Biblia inamaanisha nini inaposema upendo huvumilia? Mstari wa 4 \_\_\_\_\_

3. Ikiwa upendo 'hauhusudu, unataka nini kutoka kwa wengine? Mstari wa 4 \_\_\_\_\_

4. Ikiwa upendo hautafuti mambo yake, unatafuta nini hasa? Mstari wa 5 \_\_\_\_\_



Ni tabiasifa gani kati ya hizi unazohitaji kuzifanyia kazi zaidi? \_\_\_\_\_

Fikiri ni kwa namna gani sifa hizi zinakugusa.

5. Orodhesha tabia za upendo kutoka 1 Wakorintho 13:4-7 zinazokinzana na makosa yafuatayo.

\_\_\_\_\_ Sitamsamehe kwa kile alichonifanyia.

\_\_\_\_\_ Kwanini Jane anafahamika zaidi wakati na mimi nimefanya mambo mengi kama yeye tu?

\_\_\_\_\_ Wadogo zangu wamenishinda kabisa. Kila mara wanansumbua.

\_\_\_\_\_ Mume wangu hana maana. Hawezi kufika popote pale. Hawezi kufika popote pale.

\_\_\_\_\_ Kwa nini nimsaidie Pete wakati mwenyewe nina mahitaji ya kuyashughulikia?

\_\_\_\_\_ Kundi letu la kuabudu ni bora kuliko lao. Hawawezi hata kubeba ngoma.

\_\_\_\_\_ Sihataji msaada wa yejote yule kukamilisha mambo yangu.

\_\_\_\_\_ Ha! Wamemfukuza kazi John. Hata hivyo sikua nampenda.

\_\_\_\_\_ Naombea wamfukuze ili niichukue nafasi yake.

\_\_\_\_\_ Kila kitu kuhusu Martha kinanikera, hata anavyovaa.

## WIKI HII


Nyimbo za Kikristo ni nyenzo yenyewe nguvu sana inayoweza kutusaidia kukua. Wiki hii jifunze wimbo wenye maneno yanayohusiana na upendo miongoni mwa Wakristo wenzako.

**Ni mlengo  
gani ambao  
maisha yako  
yanauchukua?**



**Ni rahisi  
kupotea  
njiani, kuupenda ulimwen-  
gu na kile unachokitoa  
badala ya kumpenda jirani  
yako. Upendo ni kama dira  
ambayo inaweza kuturudi-  
sha katika njia sahihi.**

**Tunagombana na wengine  
pale tunapotoa kipaum-  
bele katika kupata vitu  
badala ya kujenga mahu-  
siano mazuri na watu.**



## KUWA IMARA

**Wiki hii soma  
Waebrania 11-12 na  
1 Petro 1-5**  
(sura moja kwa siku).

## Kariri Yohana 13:35.

**"Hivyo watu wote watatam-  
bu ya kuwa ninyi mmekuwa  
wanafunzi wangu, mkiwa na  
upendo ninyi kwa ninyi."**

## KUISHI PAMOJA KWA UPENDO

6. Warumi 12:10 inatuambia tujitoe kwetu sisi kwa sisi katika upendo wa kindugu. Hii ni pamoja na nini, kwa mujibu wa sehemu ya mwisho ya mstari? \_\_\_\_\_

7. Soma Wagalatia 5:14-16. Pamoja na amri ya kuwapenda majirani zao, baadhi yao wanafanya nini? Mstari wa 15 \_\_\_\_\_

Paulo alimaanisha nini aliposema "kuumana" na "kulana"? \_\_\_\_\_

Tunawezaje kushinda tamaa ya kuwaharibu wengine? Mstari wa 16

Angalia Hatua ya 5 katika Toleo la 1 kuititia kuna maana gani kutembea katika Roho.

8. Upendo unaweza kutusaidiaje kuishi pamoja? 1 Petro 4:8 \_\_\_\_\_

Elezea maana ya "upendo husitili wingi wa dhambi." \_\_\_\_\_

**Upendo wa kweli hautegemei tabia za wengine; badala yake,  
unapenda tu pamoja na makosa yaw engine. Kristo aliyatoa maisha  
yake kwa yenyewe haki na wasio haki. Sadaka yake ni mfano wa  
namna ya kupeana kwa kujitoo kwa kuhudumiana sisi kwa sisi.**

9. Soma habari ya Petro katika Yohana 21:15-17. Hata kama Petro alimkana Kristo mara tatu, Yesu alimpa kazi gani? \_\_\_\_\_

10. Taja kitu ambacho hatupaswi kukipenda. 1 Yohana 2:15 \_\_\_\_\_

11. Kwa mujibu wa Yakobo 4:1-2, nini chanzo cha vita nyingi? \_\_\_\_\_



**Kupenda mambo ya ulimwengu kunaathiri uwezo wetu wa kuper-  
dana. Tunagombana na wengine tunapotoa kipaumbelea katika kuj-  
kusanya vitu badala ya kujenga mahusiano mazuri na watu. Je kuna  
mambo yanayokinga uhusiano wako na watu wengine? Yaorodheshe.**

12. Kama Wakristo, tunapendana, lakini ni aina gani ya ukaribisho tunao-  
paswa kuutegemea kutoka kwa watu wasio waamini? 1 Yohana 3:13

Kwanini? Mstari wa 12 \_\_\_\_\_

Hata kama watu wengi wasio waamini wanatudharau na hata kutu-  
chukia, bado tunahitaji kuwapenda, kuwaombea na kuwashirikisha  
habari njema, kama vile Yesu alivyofanya.

## Hatua ya 4

# Kutiana Moyo



### KWELI AU SI KWELI

- \_\_\_\_\_ Kuwa na muda na waamini wengine kunapaswa kutuhamasisha kuwa watu wema zaidi
- \_\_\_\_\_ Ni matendo yetu tu, na si maneno yetu, yanayoweza kuwatia moyo wengine.
- \_\_\_\_\_ Mtu anapokua anapitia wakati mgumu, moja ya njia bora ya kumtia moyo ni kupata muda wa kua nae

*"Nisifie, na naweza nisikuamini. Nikosoe na naweza nisikupende. Nidharau, na naweza nisikusamehe. Nitie moyo na sitakusahau."<sup>3</sup>*

### TIANENI MOYO NINYI KWA NINYI

1. Ni amri gani mbili zinazopatikana katika 1 Wathesalonike 5:11? \_\_\_\_\_  
na \_\_\_\_\_.
2. Ikiwa tunataka kumtia moyo mtu, je ni lazima tuseme mambo mazuri tu yanayowahusu, hata kama si ya kweli? \_\_\_\_\_
3. Nini kusudi kubwa la kukutana na waamini wengine, kwa mujibu wa Waebrania 10:24? \_\_\_\_\_
4. Je aina hii ya kutiana moyo ina maanisha tunapaswa kusema mambo mazuri tu? Kwanini? Mstari wa 25  
\_\_\_\_\_
5. Ni amri gani mbili zinazopatikana katika Waebrania 10:25? \_\_\_\_\_
6. Kukutana na waamini wengine ni pamoja na kuhudhuria kanisani. Ni pamoja na ibada za katikati ya wiki, kupigiana simu, kutembeleana, kukutana katika vikundi vidogo. Ni kwa namna gani mawasiliano haya yanaweza kutusaidia? \_\_\_\_\_



Ni mara ngapi unakutana na waamini wengine? \_\_\_\_\_

Muulize mchungaji wako ikiwa kuna kikundi kidogo ambacho unaweza kujiunga.



7. Kuna umuhimu wa kukutana kwasababu tunaiona "siku ikikaribia." Mstari wa. 25. Ni siku gani mwandishi anayoizungumzia? Mstari wa. 37 \_\_\_\_\_

### NI JINSI GANI TUNAWEZA KUTIANA MOYO


8. Ni njia gani moja tunayoweza kuwatia moyo wengine? Mithali 12:25 \_\_\_\_\_
9. Soma Mithali 18:21. \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_ huwa katika uwezo wa ulimi. Maneno yana nguvu, yana uwezo wa kuinua roho zetu au kuziua. Mithali 16:24 inaongeza kwamba maneno yapendezayo ni kama sega la asali; Ni tamu nafsini, na afya katika miili yetu. Angalia "Maneno ya kutia moyo" katika ukurasa unaofata.
10. Maneno yetu yanapaswa \_\_\_\_\_ Waefeso 4:29

## MANENO YA KUTIA MOYO

1. Tumia maneno ya kusifia, kutia moyo na ya shukrani kama vile: "Safi sana", "Unaweza", "Nakuamini", "Umejitoa kadiri ya uwezo wako; usijali kuhusu makoza", "Asante kwa msaada wako."
2. Watendee wengine kwa heshima na utu. Tarajia yaliyo mazuri na sio mabaya kwa wengine. Waamini.
3. Epuka kukosoa, kuwakaripia au kuwadharau wengine. Usitarajie ukamilifu. Epuka mizaha na kashfa kwa wengine. Punguza "lakini" ("umefanya vizuri, lakini...")
4. Sikiliza kwa makini wakati wengine wanapozungumza. Wape usikivu wako wote, ukiwangalia machoni, bila kuwaza utawajibu nini watakopaliza. Usiwakatishe. Usiwahukumu. Wengine watajua kama umewasiliza ikiwa utaweza kurudia wasiwasi wao kwao.
5. Chukua wasiwasi wao kwa dhati, na wasaidie kuushinda wasiwasi huo.
6. Wafundishe kupunguza misemo kama "siwezi"
7. Chukua ndoto zao na matarajo yao kwa dhati

## FIKIRI JUU YA HILI

Tunapaswa kufanya nini tunapokutana pamoja na waamini wengine? Ni sehemu gani ya huduma inayokutia moyo? Je kuna sehemu zinazokuvunja moyo au kukuudhi? Ni zipi hizo? Zungumza na mchungaji wako, umuombe ushauri juu ya namna na kushughurika na hasira zako.



## KUWA IMARA

**Soma Mwanzo 1-7**  
(sura moja kila siku).

**Kariri 1 Wathesalonike 5:11**

"Basi, farijianeni na kujenga-na kila mtu na mwenzake, vile vile kama mnayofanya"

1. Toa mfano wa maneno yanayotia moyo na kuwajenga wengine:

---

---

Toa mfano wa maneno yanayowavunja moyo wengine: \_\_\_\_\_

---

---

**Pima Maneno yako.** Maneno yako mara nyingi:



- Hujenga    Kosoa na kemea    Fariji    Hamasisha umoja  
 Lalamika na Kunung'unika    Majungu na kuteta  
 Huinua roho za wengine

Angalia "Maneno ya kutia moyo" katika kisanduku kilichopo mkono wa kushoto.

12. Ni njia gani moja ya kuwatia moyo wengine? Warumi 12:15

Uwepo wetu pembeni mwa mtu anaepitia wakati mgumu ni wa muhimu zaidi kuliko kile tunachoweza kusema.



Tunapohuzunika na mtu, tukishirikiana nae maumivu na furaha yake, anajua kwamba kuna mtu anaemjari.

13. Paulo aliandika kuhusu unyakuo katika 1 Wathesalonike 4:13-18 ili kwamba Wakristo waweze kutiana moyo. Huu ni moja wa mfano wa namna gani Biblia inaweza kutumika kama nyenzo yenye nguvu katika kutiana moyo. Kiuhalisia ni nguvu ya Mungu. Tunaposhindwa kusikiliza na kulisoma neno la Mungu, tunajiondoa wenyewe katika uwezekano wa kupokea msaada huo.

Orodhesha vifungu kadhaa ambavyo vimekutia moyo hivi karibuni.

14. Ni maneno gani ya kutiana moyo tunayoyapata katika vifungu vifuatavyo?

1 Petro 5:7 \_\_\_\_\_

1 Yohana 4:4 \_\_\_\_\_

15. Kwa mujibu wa Waebrania 4:14-16, kuna mtu ye yeyote anaewela mahitaji yetu? \_\_\_\_\_

Tufanye nini basi? Mstari wa.16 \_\_\_\_\_

"Kiti cha neema" kinamaanisha uwepo wa rehema wa Mungu. Kupitia maombi, tunamuendea wakati wowote, tukijua kwamba Anatusubiri kutusikiliza, hata pale tunapojisikia hatufai. Biblia imejaa vifungu vyaa kutia moyo kama hiki. Vitumie ipasavyo katika kujitia moyo na kuwatia moyo wengine.



Je umekata tamaa; au unamfahamu mtu anaehitaji kutiwa moyo  
**2 katika Toleo la 1 inayozungumzia "Mimi ni nani katika Kristo"**

# Hatua ya 5

## Kutumikiana



### KWELI AU SI KWELI

- \_\_\_\_\_ Utumishi ni kwa wale tu wenye muda.  
\_\_\_\_\_ Unyenyekevu ni kanuni ya utumishi.  
\_\_\_\_\_ Viongozi mahiri ni wale wanaotafuta namna ya kuwatumikia wengine.

### KUTUMIKIA AU KUTUMIKIWA?

1. Soma Wagalatia 5:13. Hata kama tu huru katika Kristo, baadhi wanatumia uhuru huo kuruhusu shauku zao kutawala. Wanatumia vibaya neema na msamaha wa Mungu, kuutumia uhuru wao kama kisingizio cha kufanya chochote wanachokitaka. Badala ya kutumia vibaya uhuru wetu, tunapaswa kufanya nini? \_\_\_\_\_

2. Injili inatutaka tusiwe wabinafsi, lakini tuwe watumishi. Kwanini? Mstari. 14 \_\_\_\_\_

**Watumishi huuliza:** Naweza kuwafanya nini wengine?


**Watu wabinafsi** wanauliza: Watu wanifanyie nini?

Upendo na utumishi ni vitu visiviyoweza kutenganishwa. Upendo hutushawishi kutumikia, wakati utumishi huonesha upendo wetu.

*Njia ya kuelekea  
mafanikio inapitia  
katika bonde la  
utumishi.*

3. Eleza kwa ufupi kile Mathayo 20:226-28 inachotufundisha kuhusu utumishi.
- 
- 

4. Tufanye nini ili kuyafurahia maisha zaidi? Unaweza kumwambia nini yule mtu ambae ye ye anajali maslahi yake tu? \_\_\_\_\_
- 



*Wabinafsi mara zote  
wanajifikiria wao tu.*

*Wakati wa Mapinduzi ya Marekani mtu mmoja akiwa amevaa nguo za kiraia alilipita kundi la askari lililokuwa likikarabati uzio mdogo wa kujihami. Kiongozi wao alikua akipayuka tu na maelekezo pasipo kujaribu hata kuwasaidia. Kiongozi huyu alipoulizwa na mpita njia yule, alijibu kwa majivuno ya hali ya juu, "Bwana, mimi ni kopro (cheo katika jeshi)!"*

*Jamaa huyu mpita njia akaomba radhi, akashuka katika usafiri wake, na kuwasaidia wanajeshi wale walikoua wamechoka. Kazi ilipomalizika, akamgeukia yule kopro na kumwambia "Bwana kopro, wakati mwagine utakapokuwa na kazi kama hii na hau-na watu wa kutosha kuifanya, nenda kwa amiri jeshi mkuu, na mimi nitakuja kukusaidia tena." Bwana huyu hakua mtu mwiningine bali George Washington.<sup>4</sup>*

### KUJIFUNZA KWA MIFANO YA WENGINE

5. Yesu alifanya nini katika Yohana 13:3-5? \_\_\_\_\_
6. Nyakati hizo, kuosha miguu ya wageni ilikuwa ni kazi ya watumishi, chini kabisa ya hadhi ya mtu wa muhimu kama Yesu. Yesu alikua anajaribu kuwafundisha nini wanafunzi wake kwa kuosha miguu yao?  
Yohana 13:14-16 \_\_\_\_\_

Lavar os pés naqueles dias era trabalho do servo.

7. Ni mtazamo gani ambao Yesu aliuonesha ambao tunapaswa kuufuata? Wafilipi. 2:5-8 \_\_\_\_\_

Ikiwa Yesu alijinyenyekeza ili awatumikie wengine, tuna sababu ya kufanya chini ya hapo?

8. Filipenses 2.3 - 4 nos explica como servir. O que faz um servo?  
Mstari. 3 \_\_\_\_\_  
Mstari. 4 \_\_\_\_\_

## FIKIRI JUU YA HILI

Shoka imetengenezwa kwa ajili ya kazi ngumu. Hata kama inapungua kadiri inavyotumika na kunolewa, bado inatumikia kusudi iliyotengenezwa kwalo.

Kwa upande mwingine, shoka iliyoachwa nyumbani bila kutumika inakuwa ni ya huzuni, kwasababu inapata kutu haraka.

Ni bora kujitoa kuwatumikia wengine badala ya kutaka kukaa na kutafuta kile kili-cho bora kwetu sie tu. Siku utakapoiona shoka au kifaa kingine, fikiri juu ya hili.



*"Sijui nini hatma ya maisha yako, lakini kitu kimoja ninachokijua ni kwamba: watu pekee mionganini mwenu ambao watakua na furaha kweli kweli ni wale ambaao wametafuta na kupata namna ya kutumikia."<sup>5</sup>*

## KUWA IMARA

**Soma Zaburi 25-31**  
wiki hii (sura moja kwa siku).



## Kariri Wagalatia 5:13.

*"Maana ninyi, ndugu, mliitwa mpate uhuru; lakini uhuru wenu usiwe sababu ya kuufuata mwili, bali tumikianeni kwa upendo."*



Toa mifano ya namna gani unavyoweza kujali zaidi maslahi ya wengine.

9. Kwa mtume Paulo, aina ya utumishi mkuu kuliko wote ilikuwa ni kubeba habari njema ya wokovu kwa wengine. Ndio maana alisema katika Warumi 1:16, "Siionei haya injili...." Tunajifunza nini kutoka kwake katika vifungu vifuatavyo kinachowezza kutusaidia kuwatumikia wengine?  
2 Wakorintho. 4:5 \_\_\_\_\_  
2 Wakorintho. 6:3 \_\_\_\_\_
10. Ni tabia gani nyingine za mtumishi tunazoziona katika 2 Wakorintho 11:29?  
\_\_\_\_\_

## SI RAHISI, LAKINI NI JAMBO LINALOSTAHILI KUFANYWA

11. Utumishi unaweza kuwa ghari. Elezea kwa namna gani. 2 Wakorintho 6:4-8  
\_\_\_\_\_

Angalia 2 Wakorintho 11:24-28 kwa maelezo zaidi juu ya sadaka ambayo mtume Paulo aliitoa ili kuwatumikia wengine. Angalia pia 2 Timotheo 2:10.

12. Je sadaka hizo ambazo utumishi huhitaji zinastahili kutolewa? Kwa nini?  
2 Wakorintho 9:6 \_\_\_\_\_

Waebrania 6:10 \_\_\_\_\_

13. Utumishi umeelezewaje katika 2 Wakorintho. 8:4? \_\_\_\_\_

## KUFANYA VITENDO

*"Ni kazi gani ambayo Kristo aliwapatia watumishi wake kufanya? Namna ambayo wanatumikia yeye, anawaambia, ni kwa kuwa watumwa wa watumishi wenzao na kuwa tayari kufanya chochote kile, hajjalishi kinagharibu kiasi gani, kinaumiza kiasi gani, au kina thamani gani, chochote kile wanachopaswa kufanya kuwasaidia watumishi wenzao."<sup>6</sup>*

Zaidi ya yote, utumishi unakua halisia pale tunapotoa muda wetu, mali zetu na nguvu zetu.

- Kusikiliza
- Kutia moyo wengine
- Kushauri
- Kutembelea wengine
- Kufariji
- Kutengeneza mlango, gari.
- Kufyeka majani
- Kupaka rangi
- Kumtia moyo mtu kwa tabasamu.
- Kuosha vyombo
- Kumfundisha mtu kusoma
- Kumfundisha mwamini mpya
- Kumsaidia mtu na kazi zake za shule
- Kufua, kunyoosha, kushona nguo
- Kumsaidia mtu na kazi zake za siku
- Kumsindikiza mtu kwa daktari
- Kumsindikiza mtu mahali/ au kukaa na mtu mahali
- Kufanya kazi kwenye kompyuta
- Kumfundisha mtu jinsi ya kutumia kompyuta
- Kupika/kuandaa chakula
- Kubeba takataka
- Kuwaeleza watu habari za Yesu
- Kuangalia watoto wazazi wao wanapokua hawapo
- Kufundisha
- Kusafisha nyumba
- Kuomba au kumwombea mtu
- Kumsomea mtu kitabu
- Kumuzimisha mtu kitabu
- Kumpigia mtu simu na kumjulia hali



**Jiulize: "Nawezaje kuwa msaada kwa mtu leo?"**

# Hatua ya 6

## Kuvumiliiana



### KWELI AU SI KWELI

- \_\_\_\_\_ Tukiwa kama Wakristo, ni lazima tuvumilie aina zote za udharirishwaji.
- \_\_\_\_\_ Tunaweza kujifunza kuavumilia wengine kwa kuwasamehe.
- \_\_\_\_\_ Kabla ya kuwakosoa wengine, ni lazima tukumbuke kwamba sisi pia tuna mapungufu yetu.

*".....mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa; kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu, mkichukuliana katika upendo." Waefeso 4:2*

### KUISHI KATIKA ULIMWENGU HALISI

Je inakukera kuishi na mtu asiyé mkamilifu na anaedhi nyumbani au kanisani kwako/ Waefeso 4:2 inazungumza juu ya "kuvumiliiana sisi kwa sisi katika upendo" Tafsiri zingine zinasema "kujizuia" au "kuonyesha uvumilivu." Lengo ni kwamba ni lazima tujifunze kuishi na mapungufu ya wengine. Tunapoacha kulalamika juu ya mapungufu yao, tunaweza kuanza kuwapenda.

1. Mithali 19:11 inatusaidia kuelewa dhana ya "kuvumiliiana sisi kwa sisi" inaposema:

Busara ya mtu ni \_\_\_\_\_.

2. Kwa mujibu wa Waefeso 4:2, tunapaswa "kuvumiliiana sisi kwa sisi" kwa mtazamo wa: \_\_\_\_\_, \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_.

Hii itatusaidia kuwa na \_\_\_\_\_ katika kanisa. Waefeso 4:3

3. Kwanini unyenyekevu ni muhimu katika kuvumilia mapungufu ya wengine?

Mathayo 7:3 \_\_\_\_\_

4. Sote tuna mapungufu ambayo wengine lazima wavumiliane nayo. Unadhani yapi ni baadhi ya mapungufu yako ambayo yanaweza kuwa yanawakera wengine?

\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

5. Nini hatma ya familia yako ikiwa hutaweza kujifunza kuishi na mapungufu ya kila mmoja? \_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

6. Unadhani itakuathiri kwa kiasi gani ikiwa utagundua kwamba mwenzi wako hawezi kuishi na mapungufu yako na kila mara anataka kukubadirisha? \_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

7. Unadhani inawaathiri kiasi gani watoto kujua kwamba wazazi wao mara zote wanakatishwa nao tamaa kwasababu si wakamilifu?

\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_



### Wapenda ukamilifu

Je wewe ni mtu unayependa ukamilifu au unaishi na mtu wa namna hiyo? Tafakari kauli zilizopo mkono wa kulia juu ya ukamilifu katika mahusiano yetu binafsi.

*Tukiwa kama watu wakamilifu, tunawadharau wale ambao hawafikii viwango vya mategeremo yetu. Tunapotarajia mambo makubwa sana kutoka kwa wengine, tunawatwisha mizigo ambayo hawataweza kuibeba.*

*Majibu yao yanaweza kuwa ya hasira, a kukatishwa tamaa. Hajarishi ni kwa kiasi gani watajithidi kufikia viwango vyetu, sote tutaishia kuudhika tu au kukasirikiana.*

*Hatuwezi kuwa na mahusiano mazuri na wengine hadi pale tutakapojifunza kuwakubali jinsi walivy.*





*Je, tuko hapa  
kuwahudumia au  
kuwakosoa wengine?*

*Kuna mtu aliwahi  
kumwambia  
John Wesley,  
"Kamwe sisamehe na  
kamwe sisahau"  
Ambapo Wesley alijibu,  
"Bwana, basi natumaini  
kamwe hutendi  
dhambi pia."*



### KUWA IMARA

**Soma Mwanzo 8-14**  
(sura moja kwa siku).

### Kariri Waefeso 4:2

*"....mwenende kama  
inavyoustahili wito wenu  
mlioitiwa; kwa uny-  
enyeketu wote na upole,  
kwa uvumilivu, mkichu-  
kuliana katika upendo"*

8. Unadhani njia sahihi ya kuwahamasisha wengine ni kuwaabisha wanapokua wameshindwa? \_\_\_\_\_ Kwanini? \_\_\_\_\_

*Aibu mara zote hutoa matokeo, lakini si yale tunayoyataka. Inatuhamasisha ku-fanya vitu sahihi kwa sababu zisizo sahihi na inafanya kazi pale tu panapokua na mtu anaetusimamia.*

9. Je, inabidi tukubali tu tabia mbaya za wengine pasipo kuwawajibisha?

Wagalatia 6:1 \_\_\_\_\_

10. Je, staha maana yake ni kwamba watu hawatawajibika kwa matendo wanayoyafanya? Warumi. 12:17-19 \_\_\_\_\_

11. Soma Warumi 15:1-2 na jibu maswali yafuatayo:

\_\_\_\_\_ Kweli ama Si Kweli? Kuwavumilia wengine ni ishara ya udhaifu, ikionesha kwamba hatujui namna ya kujilinda. Mstari wa. 1  
Kusudi la kuvumiliana sisi kwa sisi ni \_\_\_\_\_ mstari wa. 2

Maana kuu ya kifungu hiki ni kwamba tunapaswa:

- Kuwatia moyo wengine badala ya kufanya tu kile kilicho na manufaa kwetu
- Kuwavumilia wengine hata kama hatutaki.



*Ni kweli kwamba mapungufu ya wengine yanatukera, lakini je, tuko hapa kuwatumikia au kuwakosoa? \_\_\_\_\_*

*Hebu fikiri ni kwa namna gani dhana hii inaweza kubadirisha  
maisha yako*

12. Soma Wakolosai. 3:13. Kuvumiliana sisi kwa sisi, ni lazima \_\_\_\_\_

Je, tunaweza kuvumilia mapungufu ya wengine pasipo kuwasamehe? \_\_\_\_\_  
Kwa nini? \_\_\_\_\_

Ni nani wanaoweza kuwa mfano mzuri wa msamaha kwetu? \_\_\_\_\_  
Kristo aliwasamehe wengine kiasi cha kutowahesabia hukumu adui zake wakati akiwa bado ananing'inia msalabani.

13. Wakolosai 3:8 inatuhimiza kuachana na hasira zetu. Nini hutokea pale tunapokataa kuachilia vinyongo vyetu? Je tunakua bora au wenye uchungu?

14. Ni tabia gani zingine zinazoweza kutusaidia kuvumilia maudhi ya makosa ya wengine? Wakolosai. 3:12 \_\_\_\_\_

15. Ni nani anashinda pale ambapo waumini wa kanisa wanashindana?

- Hakuna       Kundi linalokuja juu       Shetani

Ni nani anashinda katika kanisa ambalo waumini wake wanajifunza jinsi ya kuchukuliana wao kwa wao? \_\_\_\_\_

16. Kulingana na ulichoifunza katika somo hili, una maoni gani kwa wale wanaotafuta kanisa "lisilo na kasoro"? \_\_\_\_\_

## Hatua ya 7

# Msameheane



### KWELI AMA SI KWELI

- \_\_\_\_\_ Maandiko yanatuambia tusamehe wengine haijarishi wametutendea nini.  
\_\_\_\_\_ Kuweka kinyongo kutatusabishia kunaswa katika mtego wa uchungu.  
\_\_\_\_\_ Rafiki hujifunza namna ya kutoiangalia tabia ya maudhi ya rafiki zake.

1. Kwa mujibu wa Wakolosai 3:13, tunapaswa kufanya nini tunapokua na tatizo juu ya mtu?

Ni muhimu kukumbuka kwamba msamaha unahusiana na "kuvumiliana sisi kwa sisi," ikizingatiwa kwamba yote hayo ni muhimu katika kutusaidia kuishi kwa amani mionganoni mwetu. Tunahitaji kumuan-galia Kristo kama mfano wa msamaha.

2. Nini tabia moja wapo ya rafiki? \_\_\_\_\_ Mithali 17:9

"Kufunika kosa" kuna maana pia kusamehe au kutoliangalia kosa. Kifungu hicho kinarudia kwamba "jambo" linaweza kuwa ni majungu juu ya dhambi za wengine, au kukazania "jambo" hilo hilo kwa muda mrefu, na kuwakumbusha mara kwa mara juu ya mapungufu yao.

*Kutoka kifungu juu ya mwanamke aliyekamatwa akizini (Yohana 8:3-11), tunajifunza kwamba msamaha haimaanishi kwamba kuidharau dhambi. Baada ya kumsamehe mwanamke yule Yesu alimwambia nenda na usitende dhambi tena.*



3. Ni mambo gani ya mbadala kwa msamaha yanayotajwa katika Waefeso 4:31? \_\_\_\_\_

Uamuzi wako wa kusamehe au kutokusamehe utabashiri hatma ya maisha yako. Una chaguzi mbili tu – kusamehe au kuwa na uchungu. Kutafuta kulipiza kisasi kutakupelekea kujuta tu. Chagua kuachilia hasira yako.



Tafakari mawazo yafuatayo:

"Kubeba kinyongo ni sawa na kutungwa na nyuki hadi kifo." <sup>7</sup>

"Msamaha haubadirishi yaliyopita, lakini inapanua siku za usoni." <sup>8</sup>

Unachagua mtindo gani wa maisha?  Uchungu — kung'ang'ania kinyongo  Amani — kusamehe

4. Waefeso 4:32 inaoanisha msamaha na moyo wa huruma. Kwanini vinaenda pamoja? \_\_\_\_\_

Msamaha ni matunda ya moyo wa huruma.

5. Tunapaswa \_\_\_\_\_ dhambi zetu sisi kwa sisi na \_\_\_\_\_ sisi kwa sisi. Yakobo 5:16.

Kukiri dhambi zetu kwa wengine si jambo rahisi. Baadhi ya mambo yanayoweza kutuzuia kukiri ni pamoja na hofu ya kudhihakiwa, kiburi, hofu ya kwamba watu watajua kile tulichofanya, nk. Mambo gani mengine yanayoweza kutuzuia kukiri dhambi zetu \_\_\_\_\_

6. Roho ya kukosoa hufanya kusamehe wengine kuwa kazi ngumu. Biblia inasema nini kuhusu kukosoa?


Warumi 2:1 \_\_\_\_\_

Matthayo 7:1-5 \_\_\_\_\_

## KUWA IMARA

### Soma Mwanzo 15-21

wiki hii (sura moja kwa siku).



### Kariri Waefeso 4:32

"....tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenyewe huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.."

## HADITHI ZA MSAMAH

- Baada ya vita, Ribert E Lee alimtembelea mwanamke mmoja wa mji wa Kentucky ambaye alimpeleka katika mabaki ya mti wa zamani sana mbele ya nyumba yake. Walipofika pale, mwanamke yule alilia kwa uchungu sana kwamba matawi na shina la mti ule uliharibiwa na moto. Akamwangalia Lee ili angalau asikie akiwakemea wahusika au basi hata neno la faraja kwa kuupoteza mti ule.

Baada ya ukimya mfupi, Lee alisema, "Mpendwa, kata kila kilichobakia, na sahau kabisa." Ni bora kusamehe dhuruma iliyopita kuliko kuruhusu ibaki, chuki isije ikaota mizizi ndani yako na sumu ikatawala maisha yako.9

- Kuna hadithi ya Kihispania ya baba na kijana wake waliokosana. Yule kijana akakimbia, na baba akaamua kwenda kumtafuta. Alimtafuta kwa miezi mingi bila mafanikio. Hatimaye, katika hatua za mwisho karibu na kuktata tama, baba yule alitoa tangazo katika gazeti la Madrid. There's a Spanish story of a father and son who had become estranged.

Tangazo lile lilisomeka: "Mpendwa Paco, tukutane mbele ya ofisi za gazeti hili siku ya jumamosi jioni. Nimekusamehe yote. Nakupenda. Baba yako.

Siku ya Jumamosi wakina Paco wapataao 800 walienda kwenye ile ofisi, wakitafuta msamaha na upendo kutoka kwa baba zao.10

Kwa taarifa zaidi juu ya msamaha, angalia hatua ya 7 na 8 katika Toleo la 2 la Maisha Mapya ndani ya Kristo. Unaweza kupata pia Toleo hilo la 2 katika [www.NewLifeDiscipleship.com](http://www.NewLifeDiscipleship.com).

Kwa kifupi, nini tatizo kuu juu ya kuwahukumu wengine? \_\_\_\_\_

7. Ni nani kati yetu ana haki ya kuwahukumu wengine? Matthayo 7:5

*Biblia inatuamuru kuwasamehe wengine, hajalishi wamefanya nini. Tunawasamehe hata adui zetu. Hii haimaanishi kwamba mkosaji hatawajibishwa kwa alichokifanya. Pande zote zina wajibu:*

- **Mkosaji** ana wajibu wa kutubu na kuomba msamaha.
- **Mkosewaji** ana wajibu wa kusamehe, hata kama hadhani kwamba yule mtu anastahili msamaha. Anaposamehe, anakuwa amefanya kile anachopaswa kufanya na anakuwa huru kuachana na uchungu uliokuwa ukiyaendesha maisha yake.

8. Ni aina gani ya tabia tunazoweza kuzitaraja kutoka kwa watu wa Mungu?

Mithali 24:17 \_\_\_\_\_

Mithali 24:29 \_\_\_\_\_

Kutoka 23:4-5 \_\_\_\_\_



*Hebu jaribu kufikiria mfano wa nyakati hizi unaofanana na Kutoka 23:4-5 ambao unaweza kuanza kuufanya kazi leo*


9. Ni kwa kiasi gani msamaha wetu unapaswa kwenda? Kwa mujibu wa

Luka 6:35-36, mtu anaesamehe \_\_\_\_\_, na kuwatendea \_\_\_\_\_.

Anafanya yote haya pasipo \_\_\_\_\_ (uk. 35)

Anafuata mfano wa Mungu wake, ambae ni \_\_\_\_\_ (uk. 36)

Rehema haimpatii mtu adhabu anayostahili. Kwa mfano, hutenda mema, hata kwa waovu na wasio shukrani. (uk.35).



## Mawazo juu ya Msamaha

- Msamaha si sawa na kusahau kosa. Inachukua muda kwa kumbukumbu kufutika mara baada ya kuwa nimesamehe.
- Maana yake naacha kumgombeza yule mtu, na kufukua yale yaliyo mabaya tu juu yake
- Haihitaji kisasi wala adhabu, kwasababu naelewa kwamba mkosaji atapaswa kujibu mbele za Mungu kwa kile alichokifanya.
- Msamaha kimsingi ni uamuzi wa kuachia hasira zangu. Hata kama sitaki kusamehe, ni namna pekee ya kuiweka huru kutoka uchungu.
- Uamuzi wangu kusamehe hautegemei na mtazamo au vitendo vya mtu alienikosea.
- Kumbukumbu mbaya zitakaponijia katika mawazo yangu naweza kusema: "Tayari nimesamehe. Nakataa kubaki katika ya kale."

## Hatua ya 8

# Kupoakeana sisi kwa sisi



### KWELI AU SI KWELI

- \_\_\_\_ Umoja katika kanisa unatutaka kuwapokea hata watu wanaokera.
- \_\_\_\_ Ikiwa tutawapokea wasio mcha Mungu, waumini wengine watakukosoa.
- \_\_\_\_ Kuwapokea wenge dhambi ina maanisha tunakubaliana na matendo ya wenge dhambi.

Familia ya Mungu ni kubwa na inajumuisha aina zote za watu. Wengine wamekomaa na wengine hawajakomaa. Wengine ni rahisi kupatana nao, wakati wengine husababisha matatizo kila siku. Biblia inatuambia tupoakeane sisi kwa sisi. Hajalishi ni kina nani, Mungu anataka umoja mionganoni mwa familia yake.

### KUISHI NA WATU WANAOKERA

1. Mungu anataka nini kwa watu wake? Warumi 15:5-6 inaomba kwamba Mungu awapatie waamini \_\_\_\_\_ wanapomfuata Mungu, anaetoa saburi/uvumilivu na faraja
2. Nini kinatakiwa ili kuishi pamoja kwa amani? Warumi 15:7 \_\_\_\_\_  
Kuwapokea wengine ni kuwakubali, pamoja na madhaifu yako.
3. Je, tunaweza kuchagua ni kina nani watakuwa kaka na dada zetu katika Kristo?  Ndio  Hapana  
Je, tuna ndugu wanaotuudhi?  Ndio  Hapana  
Je, kuna waamini kanisani kwetu wenge matatizo makubwa na upungufu fulani?  Ndio  Hapana  
Hiki ndicho kitu ambacho Warumi 15:1 inachotusih \_\_\_\_\_
4. Warumi 15:8-9 inazunguma juu ya makundi mawili ya watu, Wayahudi (waliotahiriwa) na \_\_\_\_\_ (mst.9). Huko kale, Wayahudi waliwadharau sana Watu wa Mataifa, wasitake kabisa kujihusisha nao, hata kupeana nao mikono; lakini baada ya kuwa wamempokea Kristo, mambo yalibadirika. Mungu aliwafanya wote kuwa katika familia moja.  

5. Soma Luka 19:1-10 ujibu maswali yafuatayo kuhusu Zakayo:  
Zakayo alikuwa na hadhi ya namna gani? mst.2, 7 \_\_\_\_\_
6. Hata kama Zakayo hakuwa mtu mwenye hadhi ya juu, Yesu hakumbeza. Ni kwa namna gani kumkubali kwa Yesu kulimgusa Zakayo, hata kama alikuwa amekataliwa na wengi? mst.6 \_\_\_\_\_  
mst.8 \_\_\_\_\_
7. Yesu aliwajibu nini wale waliomkosoa kwa kujihusisha na wenge dhambi kama Zakayo? mst 10  





*Kanisa ni familia, lakini pia ni kimbilio na hospitali kwa watu wenge matatizo. Hospitali itakua na maana gani ikiwa itapokea watu wanaojisikia vizuri tu?* \_\_\_\_\_

*Luka 15:7 inazungumza juu ya furaha mbinguni pale mwenye dhambi mmoja anapotubu. Mungu humtafuta na kumkaribisha yule aliyepotea. Tufanye pungufu ya hapo? Ni nani anastahili kukaribishwa kanisani kwetu?*

- |   |   |   |  |
|---|---|---|--|
| <input type="checkbox"/> Watu wazuri                          | <input type="checkbox"/> Watu wanaokera | <input type="checkbox"/> Watu wa hadhi ya juu                               | <input type="checkbox"/> Wanyonge na wasiokomaa  |
| <input type="checkbox"/> Wasio waadilifu                      | <input type="checkbox"/> Wakristo imara | <input type="checkbox"/> Watu wa daraja la chini                            | <input type="checkbox"/> Walioathirika na madawa |
| <input type="checkbox"/> Walio na mitazamo ya tofauti na yetu |   | <input type="checkbox"/> Wageni na watu wenge rangi na mila tofauti na zetu |  |

## KUWA IMARA



Soma Mwanzo 22-28  
wiki hii.

### Kariri Warumi 15:1-2.

"Basi imetupasa sisi tulio na nguvu kuuchukua udhifu wao wasio na nguvu, wala haitupasi kujipendeza wenyewe. Kila mtu mionganini mwetu na ampendeze jirani yake, apate wema, akajeng-gwe."

## JAMBO LA KUZUNGUMZIA

Soma Luka 7:36-50 na jadiri mitazamo mbalimbali ya Yesu na Mafarisayo juu ya mwana-mke mwenye dhambi.

8. Ikiwa tutakaribisha aina zote za watu, je hii ina maana kwamba kanisa haliwezi kuweka viwango nya tabia/mienendo? \_\_\_\_\_  
Kwanini? \_\_\_\_\_

Kuwapokea wanyonge haimaanishi kwamba tunatakiwa tuwaache watawale au wasababishe utengano; badala yake, tunapaswa kutafuta namna ya kuwajenga (Warumi. 15:1-2).



*Utafanyaje kuwafanya watu wa aina hii wajisikie vizuri kanisani kwako?  
Fikiri watu dhahiri kabisa ambao labda wapo kanisani kwako.*

- Wanyonge na wakimya \_\_\_\_\_
- Wageni: \_\_\_\_\_
- Watu wenye matatizo: \_\_\_\_\_

*Por exemplo, convidar para tomar um café, jantar, orar.*

9. Ni matatizo gani Yakobo 2:1-4 inayaonesha? \_\_\_\_\_

Tunaweza kujifunza nini kutoka katika kifungu hiki? \_\_\_\_\_

Ni kinyume gani kinachotolewa katika mstari wa 5-7? \_\_\_\_\_

Si hivyo tu, lakini mara nyingi hawa watu wakimya na wanyonge ambao labda hawatuvutii kwa mara ya kwanza mara nyingi wanakuwa watu wazuri zaidi kuliko hata hao tunaowaona kama "watu wa muhimu"

10. Waefeso 4:3-4 inatuamuru kuwa \_\_\_\_\_. Tunaweza kuungana ikiwa hatuwapokei wau-mini wengine kama jinsi walivyo?  Ndio  Hapana

## INAYOSTAHILI HESHIMA

11. Ni aina gani nyingine ya watu tunaohitaji kuwapokea? Wafilipi 2:25, 29 \_\_\_\_\_

Tunapaswa kuwatendea vipi watumishi wa Mungu? mst.29 \_\_\_\_\_

**STOP** *Utafanyaje kuheshimu viongozi wa kanisa lako?* \_\_\_\_\_

### Neema au Sheria?

Waamini wengi wamechanganyikiwa na kukata tama, wakiwa wamefunkwa na hisia za hukumu, kwasababu wanahisi kama vile wanachungwa muda wote na Wakristo wengine. Hawasikii upendo, neema wala kupokelewa, badala yake ni hali nzito ya kuhukumiwa na roho ya majivuni na mitazamo ya kuijinua.

Wakati ni kweli kwamba Biblia imeweka viwango nya hali ya juu, mara nyingi huwa tunaweza tamaduni na desturi zetu juu ya viwango nya Mungu. Ni rahisi kutaka wengine waishi kwa orodha zetu za "fanya hichi, usifanye hichi" kuliko kuangalia ndani na kuona miyo yao. Labda nia zetu ni nzuri tunapowahukumu wengine, lakini hii inaitwa sheria. Haimaanishi kwamba hatuna haki ya kuonesha makosa, na kuwaacha watu wafanye chochote kile wanachokitaka. Biblia inatuambia pia kwamba tunapaswa kuwashauri wengine, lakini kwa neema na upole, tukizingatia ushauri wetu katika amri za kibiblia, na si maoni yetu binafsi.



**SHERIA**

# Hatua ya 9

## Shaurianeni



### KWELI AMA SI KWELI

- \_\_\_\_\_ Kuepuka matatizo, ni bora usitoe ushauri kwa yeyote yule.
- \_\_\_\_\_ Nikihisi Mungu ananiongoza kumshauri mtu, unapaswa kufanya hivyo bila kuchelewa.
- \_\_\_\_\_ Ushauri wangu ukitegemea Biblia bila shaka utakuwa unafaa.

### HATUWEZI KUPUUZIA

1. Waebrania 3:13 inatuamuru \_\_\_\_\_  
“Tia moyo” katika tafsiri nyingine inasema “toa ma-usia”, na tafsiri nyingine zinasema “kuonyana”
2. Ni wakati gani muafaka kuhusiana? mst. 13 \_\_\_\_\_
3. Ikiwa tutapuuzia na kushindwa kukemea dhambi, tunajihatarishia \_\_\_\_\_ kwa udanganyifu wa dhambi. mst.13. Moyo mgumu una tabia gani? \_\_\_\_\_

Kadiri mtu anavyoachwa bila kukemewa juu ya dhambi zake, ndivyo hivyo anavyoendelea kukomaa katika dhambi. Watu wengine wanadhamira zilizo hai, wakati wengine wanaonekana kupuuzia maonyo. Inachukua muda moyo kuwa mgumu, ndio maana ni rahisi sana kwa baadhi kusema: “Kuna haja gani ya kuwahi? Nitashughulika nalo kesho.”

Kwanini mara nyingi tunasubiri hadi “kesho” kabla ya kuzungumza na watu juu ya tatizo tunaloliona?



Unahisi kama Mungu anakuongoza kwenda kumshauri mtu, lakini bado hujachukua hatua yoyote ile?

Ni nini kinachokuzuia kuzungumza na mtu huyo?

Kuna sababu yoyope iliokuzuia usichukue hatua leo (wiki hii)?


Tengeneza mpango wa namna gani utamwendea mtu na kumtia moyo.

4. Kweli ama si kweli:

\_\_\_\_\_ Kumu usia mtu maana yake ni kumlazimisha mtu abadirike.

\_\_\_\_\_ Njia bora ya kumu usia mtu ni kumuaibisha hadi abadirike.

\_\_\_\_\_ Kumu usia mtu maana yake ni kumtia moyo mtu abadirishe mtazamo wake.



### JINSI YA KUWASIHİ WENGINE

5. Mtazamo wetu unapaswa kuwaje tunapewasihi watu waachane na dhambi zao? 1 Timotheo 5:1-2 \_\_\_\_\_

Je kukaripia na kuwatisha watu ni njia inayokubarika katika kusihu? \_\_\_\_\_

Tunapomsihi mtu, tunapaswa kumuheshimu, kama mmoja wa wanafamilia wenzetu. Unapofika muda wa kuzungumza na mtu jiulize: “Je, hivi ndivyo ningependa mtu amfanyie mama yangu, baba yangu au dada yangu?”

6. Kwa mujibu wa 2 Timotheo 3:16, njia yenye nguvu ya kumsahihisha mtu ni \_\_\_\_\_. Biblia inafaa kwa \_\_\_\_\_, \_\_\_\_\_, \_\_\_\_\_, na \_\_\_\_\_

## KITU CHA KUTAFAKARI

Sisi sote tunahitaji ushauri na nyakati zingine ku usiwa. Ni lazima tuwasikilize ili tujifunze kutoka kwao.

Kuna methali ya Kiafrika inasema:

**"Malezi ya mtoto yanahitaji kijiji kizima."**

Nini mantiki kuu ya methali hii?

Methali hii ina maana gani kwa Kanisa la leo?

Ninawahitaji kweli kaka na dada zangu katika Kristo ili niwe mtu ambae Mungu ananikusudia kuwa?

**"Yeyote anaetoe ushauri, hujenga kwa mkono mmoja; yule anaetoe ushauri na kuwa mfano, hujenga kwa mikono yote miwili; lakini yule anayetoe maonyo mazuri na mfano mbaya, hujenga kwa mkono mmoja na kuboma kwa mkono mwingine."**<sup>11</sup>



## KUWA IMARA

**Soma Mwanzo 29-35**  
wiki hii (sura moja kwa siku).

*Kariri Waebriana 3:13.  
"Lakini mwonyane kila siku, maadamu iitwapo leo; ili mmoja wenu asifanywe mgumu kwa udanganyifu wa dhambi"*

Mara zote kuna mtu atatuambia nini tunapaswa kufanya, lakini tutujuaje ikiwa ushauri huo unapaswa kufanyiwa kazi? Tunapotumia Biblia kuwashauri wengine, tunaweza kuamini kwamba tunawaeleza watu hekima ya Mungu, na si maoni yetu tu.

7. Ndio maana 2 Timotheo 4:2 inatutia moyo \_\_\_\_\_.

Ni wakati gani ndio mwafaka kutumia Neno la Mungu kwa ajili ya ma usia? \_\_\_\_\_

8. Hata kama tunatumia Biblia, sehemu ya mwisho ya mstari inatuambia tuwaonye na kuwasihii wengine kwa \_\_\_\_\_.

Nguvu ya kubadirisha maisha haitoki kwenye maneno yetu wenyewe, bali kutoka Neno la Mungu. Tunahitaji kuwa wavumilivu, tukifahamu kwamba Roho Mtakatifu atatumia Maandiko katika maisha ya wengine.

9. Biblia imejaa mashauri. Kwa mfano, unaaswa kufanya nini katika vifungu vifuatavyo kutoka kitabu cha Wafilipi?

1:27 \_\_\_\_\_

2:3-4 \_\_\_\_\_

3:1 \_\_\_\_\_

10. Changamoto ni njia mojawapo ya kusihi, kwa kuwashawishi wengine kuwa na mtazamo fulani na kutenda mambo fulani. Kwa mfano, tunapewa changamoto ya kufanya nini katika Mathayo 28:19-20?



*Unatarajia nini kutoka kwa wengine?*



*Nyakati zingine tunatarajia kidogo sana. Fikiri juu ya yafuatayo:*

*"Mtendee mtu kama alivyo, na atabaki kuwa hivyo hivyo. Mtendee mtu kama jinsi ambavyo anaweza kuwa na anapaswa kuwa kuwa, na atakuwa kama anavyoweza kuwa na anavyopaswa kuwa"<sup>12</sup>*

Upande mwingine wa shiringi ni kutarajia mengi kutoka kwa wengine. Tunapaswa kuepuka kutaka vingi sana kutoka kwa wengine. Kwanini?

## MARUDIO: KWELI AMA SI KWELI

- \_\_\_\_\_ Kusihi kunapaswa kumfanye mtu ajisikie mwenye hatia kuhusu dhambi zake.
- \_\_\_\_\_ Kusihi kunapaswa kumuelekeze mtu jinsi ya kufanya kile kilicho sahihi.
- \_\_\_\_\_ Ni bora kukaa kimya ili usimkosee mtu.
- \_\_\_\_\_ Mashauri yetu kwa wengine ni lazima yatokane na Maandiko, na si maoni yetu wenyewe
- \_\_\_\_\_ Tunapaswa kusihi watu kwa upole na heshima.

# Hatua ya 10

## Kuonyana



### KWELI AMA SI KWELI

- \_\_\_\_\_ Ni bora kunyamaza kuhusu dhambi ili kwamba tusikatishane tamaa.  
\_\_\_\_\_ Tunapowaonya wengine, inapaswa kuwa kwa upendo na heshima.  
\_\_\_\_\_ Kuwakaripia watu kwa nguvu ndio kunawaadabisha na kuwasaidia kuwa Wakristo imara

### UKWELI UTAMJENGA NDUGU

"...tukimwonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu katika hekima yote, tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo." Wakolosai 1:28

1. Soma Mithali 24:24-26 na ujibu maswali yafuatayo:

Ni makosa gani tunayopaswa kuyakwepa? mst. 24 \_\_\_\_\_

Kipi ni kitu sahihi kufanya? mst. 25-26 \_\_\_\_\_

Nini kinatokea tunapowaonya waovu kwa ukweli? mst. 25-26 \_\_\_\_\_

2. Tunapaswa kuuvua \_\_\_\_\_ na kuzungumza \_\_\_\_\_. Waefeso 4:25

Kuwaeleza wengine ukweli juu ya makosa yao ni njia bora ya kushughulika na matatizo yao; lakini hili linahitaji ujasiri kwasababu si watu wote wako tayari kusikia ukweli. Kuzungumza ukweli si jambo rahisi wakati wote, lakini ni kwa faida yao.

3. Hatimaye, yule ambaye \_\_\_\_\_ zaidi ya mtu anaetumia \_\_\_\_\_. Mithali 28:23

Kwanini mara nyingi tunapendelea kupendeza watu badala ya kuwakemea? \_\_\_\_\_

4. Tunapaswa kujibu vipi watu wanapozungumza nasi juu ya dhambi zetu? Mithali 28:13 \_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_. Kuficha matatizo kutasababsha kushindwa tu. Wakati kuyakabili kwa ukweli na kutubu kutatuletea msamaha na kuturuhusu kuushinda udhaifu..

5. Lengo la kuonya ni \_\_\_\_\_. Wakolosai. 1:28 Lengo hili zuri linapaswa kutushawishi kuendelea mbele, tukimwamini Mungu kuyabadirisha maisha. mst. 29

### JINSI YA KUWAONYA WENGINE

6. Ili kuwfundisha wengine ni lazima tuwe tumejaa \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_. Warumi. 15:14

Mafundisho yasiyo na wema yatakuwa ni ya namna gani/ yatafananaje? \_\_\_\_\_

Mafundisho pasipo maarifa yatakuwaje/ yatafananaje? \_\_\_\_\_

Pasipo maarifa mara nyingi tunaharibu badala ya kujenga. Tunahitaji maarifa na hekima ya kibiblia pamoja na maarifa ya jambo lenyewe ili tuweze kumuonya muhusika kwa ufasha.

7. Yakobo 1:19 inatuambia tuwe wepesi wa \_\_\_\_\_ na wazito wa \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_.

Mara nyingi hatuwasikilizi watu hadi mwisho, halafu tunawakatisha kwa ushauri au maonyo yetu, pasipo kuchukua muda na kuelewa jambo lenyewe. Tusishangae ikiwa mtu huyo atakataa mashauri yetu kwasababu anajisikia kuwa hatukumsikiliza au kwamba hatuna maarifa.

8. Katika 1 Wakorintho 4:14, Paulo hakuwaandikia Wakorintho ili \_\_\_\_\_ bali \_\_\_\_\_. kama jinsi \_\_\_\_\_. Maonyo yanahitaji uimara lakini si uonevu. Kumuabisha mtu kutakuumbua, na kutatengeneza ngome na uasi badala ya toba.



Kumuaibisha  
mtu mbele  
ya umma  
kutatuaibisha  
sisi wenyewe,  
a kutengeneza  
mgomo na uasi  
badala ya toba.

### KWA MAFUNZO ZAIDI

Taja dhambi mbaya kabisa  
inayostahili kuonya. Tito  
3:10

Dhambi ya kusababisha  
vurugu ni mbaya kiasi gani?  
mst.10-11

Zipi ni baadhi ya mbinu  
zinazotumiwa na wafanya  
vurugu?

### FIKIRI JUU YA HILI

Tunawezaje  
kuwaonya  
wengine Warum 15:14)  
pasipo kuwa wahukumu  
(Warumi 14:13)?

Wale wanaoonya wanahitaji  
wema na ufahamu (Warumi  
15:14), lakini zaidi sana wa-  
nahitaji kujiangalia kwanza  
kuona ikiwa wanastahili  
kuwakosoa wengine (Luka  
6:41-42).

### KUWA IMARA

**Soma**  
**Mwanzo 36-42**  
(sura moja kwa siku).



### Kariri Wagalatia 6:1.

"Ndugu zangu, mtu  
akighafilika katika kosa lo  
lote, ninyi milio wa Roho  
mrejezeni upya mtu kama  
huyo kwa roho ya upole,  
ukijiangalia nafsi yako usige  
ukajaribiwa wewe mwe-  
nyewe."

### Soma Wagalatia 6:1-3 na ujibu maswali yafuatayo.

9. Ni mtu wa aina gani anayestahili kuwarekebisha wengine?

---

10. Ni katika hali gani tunapaswa kuwarudisha walioanguka? \_\_\_\_\_

Maana ya mstari wa 1 ingebadirikaje ikiwa tungeweka neno "adhabisha"  
au "kemea" badala ya "kurejesha"? \_\_\_\_\_

---

11. Ni onyo gani lingine tunalipata mwishoni mwa mstari wa 1 na katika mstari  
wa 3? \_\_\_\_\_

Hata wale walio wacha mungu zaidi kuliko wengine wanajaribiwa pia, hiyo  
hakuna nafasi ya majivuno. Ni neema ya Mungu tu ndiyo inayotuzuia tusian-  
guge.

12. Sehemu nyininge ya kumrudisha mtu ni \_\_\_\_\_ mst. 2  
"Mizigo" tunayowabebea wengine si yale matatizo ya kila siku ambayo kila  
mmoja wetu ana wajibu wa kujibebea mwenyewe. "Mizigo" inayozung-  
umzwa hapa ni yale majoribu mazito ambayo mtu hawesi kuyabeba peke  
yake. (mstari wa 5)

13. Mathayo 18:15-17 inatupa mfano wa namna ya kuishi na mtu anaetuten-  
dea dhambi. Ni hatua gani tatu ambazo lazima tuzifuate?

mst.15 \_\_\_\_\_

mst.16 \_\_\_\_\_

mst.17 \_\_\_\_\_

Ipi kati ya hatua hizi tatu ambayo ni ngumu zaidi kwako? \_\_\_\_\_

Ni mara ngapi huzitumia hatua hizi kushughurika na wale wanaotukosea

Mara zote  Mara nydingi  Si mara kwa mara  Sizitumii kabisa

14. Kwanini ni muhimu kuzungumza faragha kwanza na mkosaji? \_\_\_\_\_

Mara nydingi hutokea na ni rahisi kuiruka hatua ya kwanza na kuingia moja  
kwa moja katika majungu.

15. Kwanini tunahitaji mashuhuda wa hatua ya 2? \_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

16. Nini madhara ya kudharau ushauri wa kanisa? \_\_\_\_\_

Kuwatendea wengine kama wapagani au watoza ushuru haimaanishi  
kuwa mkatili au kuwakataa, lakini ni kuwatendea kama vile si waamini.

### REVISÃO Falso ou Verdadeiro?

\_\_\_\_\_ Kumtendea mtu vibaya kutamsaidia kukaa katika mstari ulionyooka na mwororo.

\_\_\_\_\_ Hatupaswi kuwakemea watu kabisa; badala yake, tunapaswa kuwakubali tu.

\_\_\_\_\_ Kusihii ni lazima kuwe juu ya wema

\_\_\_\_\_ Kumuaibisha mtu kutamfanya azisahau dhambi zake.

\_\_\_\_\_ Wengi hukimbilia kukosoa tu, kukaripia bila kuwa na taarifa kamili.

\_\_\_\_\_ Ikiwa tutazungumza kwa upole, mtu hataelewa ukubwa wa dhambi yake

\_\_\_\_\_ Hatua ya kwanza ya kuwaonya watu ni kwenda mbele ya kanisa moja kwa moja

\_\_\_\_\_ Ni muhimu kuyapima maisha yetu kwanza kabla ya kuwashauri wengine

# Hatua ya 11

## Salimianeni. Tendeaneni.



### KWELI AMA SI KWELI

\_\_\_\_\_ Kanisa ni mahali ambapo tunaweza kuhusiana na kuwa na ushirika na waamini wengine, na si kupokea mafunzo tu.

\_\_\_\_\_ Maneno yetu yanaweza kuwatia moyo wengine.

\_\_\_\_\_ Waamini wengi wana njaa ya uhusiano na watu wengine.

### KUSALIMIANA NINYI KWA NINYI

1. Kuna tabia nzuri sana inayoelezewa katika Warumi 16:16. Ni ipi hiyo? \_\_\_\_\_

"Busu takatifu" ilikuwa ndio njia waamini walijosalimiana kwayo enzi za kibiblia. Hata kama salamu zinatofautiana katika mila mbali mbali, "busu takatifu" bila shaka litakuwa ni salamu njema – kutoka ndani ya moyo wa mtu, lakini pia inayokubarika/ inayofaa (takatifu).

2. Kwa haraka haraka, Wakolosai 4:7-18 haionekani kuwa kifungu kinachovutia sana; lakini ukiangalia kwa makini, inatoa mwongozo mzuri juu ya namna gani tunapaswa kuhusiana na Wakristo wengine. Jibu maswali yafuatayo kwa kutumia kifungu hiki.

Kifungu hiki kimebeba nini? \_\_\_\_\_

3. Kwanini kifungu hiki kimewekwa katika Biblia? Tunaweza kujifunza nini kutoka kwacho? \_\_\_\_\_

4. Fikiri juu ya kifungu hicho, halafu amua ikiwa sentensi hizi zifuatazo ni za kweli au si kweli.

\_\_\_\_\_ Paulo aliwapenda kweli kweli waamini wa Kolosai.

\_\_\_\_\_ Salamu kama hizi ni za kujuliana hali tu, lakini pia ni za juu juu tu

\_\_\_\_\_ Ililiwa vigumu kwa Paulo kukumbuka majina ya watu.

\_\_\_\_\_ Paulo alikuwa na uhusiano wa karibu wa kichungaji na Wakristo wa Kolosai.

\_\_\_\_\_ Paulo yeye alizingatia mafundisho ya Biblia tu pasipo kujali kujihusisha na maisha ya watu.

\_\_\_\_\_ Paulo alipendelea kuwa peke yake na kwakweli alikuwa hakuwa na subira sana na wengine.

\_\_\_\_\_ Paulo alitumia salamu hizi kuwashamasisha na kuwatia moyo waamini



5. Andika baadhi ya sentensi za faraja ambazo Paulo alizitumia katika salamu zake

mst. 7 \_\_\_\_\_

mst. 9 \_\_\_\_\_

mst. 11 \_\_\_\_\_

mst. 12 \_\_\_\_\_


mst. 14 \_\_\_\_\_



Watu wanasema nini kuhusu wewe? Ni mtu unayejenga urafiki kirahisi au unajali mambo yako tu?

Jitathmini katika kipimo cha namba 1-5.

Si rafiki 1 2 3 4 5 Rafiki



*"Baadhi ya watu wanakufanya ujisikie nyumbani. Na wengine wanakufanya utamani ungekuwa nyumbani."<sup>13</sup>*

Baadhi ya watu hutumia vibaya ukarimu wetu. Hebu fikiri juu ya msemo huu tulionao kwa Kiswahili.

*"Mgeni siku ya kwanza, siku ya pili mpe jembe akalime."*



### KUWA IMARA

**Soma Mwanzo 43-50**  
(sura moja kwa siku).

**Kariri 1 Petro 4:9.**

*"Tendeaneni kwa ukarimu bila manung'unico."*

### KUTOA UKARIMU

6. Kwa mujibu wa 1 Petro 4:9, tunahitaji kuwa \_\_\_\_\_ na pasipo \_\_\_\_\_. Hata kama tunawatendea wengine vyema, sura zetu zinaonesha ikiwa ukarimu wetu ni wa kumaanisha au sivyo.
7. Ukarimu wa kumaanisha ni nini? Kujibu swalii hili, fikiri juu ya sentensi zifuatazo halafu amua ikiwa ni za kweli au si kweli.
  - \_\_\_\_\_ Ukarimu unahitaji uwezo wa kutengeneza kikombe cha kahawa kizuri.
  - \_\_\_\_\_ Ukarimu ni uwezo wa kuwafanya wengine wajisikie nyumbani.
  - \_\_\_\_\_ Ni muhimu kuwa na nyumba nzuri ili tuweze kuwaburudisha wageni.
  - \_\_\_\_\_ Ukarimu unatoka moyoni. Ni njia ya kuonesha upendo kwa wengine.
  - \_\_\_\_\_ Watu wakarimu wanawakaribisha wageni pasipo kuweka rekodi ya ikiwa watu hao wamewalipa kwa wema au lah.
  - \_\_\_\_\_ Ukarimu unahitaji roho ya utoaji, lakini pia si kutumia tu pesa nyingi.
  - \_\_\_\_\_ Penda ama usipende, tunatakiwa kuwa wakarimu.
  - \_\_\_\_\_ Kuwa wakarimu haimaanishi kwamba lazima tuwakaribishe watu nyumbani kwetu.
8. Watu wengi wanaishi maisha ya upweke, labda kwasababu hawana familia au marafiki. Hata wale wenye "marafiki" mara nyingi wanajisikia uhitaji wa kuwa na mawasiliano na karibu na wengine. Na hii ndio sababu haswa kwanini ukaribu ni wa muhimu sana, kwasababu unawasaidia watu hawa kujisikia kwamba kuna watu wanawajali na wanaopenda kujua zaidi kuhusu maisha yao. Wanakuja kanisani kumtafuta Mungu lakini pia mahusiano na watu wengine.



*Wageni wanapokelewaje kanisani kwako?*

---



---



---

*Andika namna unayoweza kuwafanya wageni wajisikie kukaribishwa kwa dhati na wajisikie nyumbani katika kanisa lako.*

---




---



---



---



Rejesho

1. 6000 Sermon Illustrations, ed. Elon Foster (Grand Rapids, MI: Baker Book House), 1992 p. 309
2. Albert Schweitzer
3. William Arthur Ward
4. Today in the Word, March 6 1991
5. Albert Schweitzer
6. James Packer in Your Father Loves You, Harold Shaw Publishers, 1986
7. William Walton
8. Paul Boese
9. Lee: The Last Years, by Charles Bracelen Flood
10. Bits & Pieces, October 15, 1992, p. 13
11. Francis Bacon
12. Goethe
13. Arnold H. Glasow

## Kiambatisho cha 1

Kata katika mistari. Tembea na kadi hizi na ukariri mistari hiyo ya Biblia

Hatua ya 4      1 Wathesalonike 5:11  
Hatua ya 8      Warumi 15:1-2.

"Basi, farijaneni na kuiengana kila mtu na mwenzake, vile vile kama mnayoofanya"

"Basi imetupasa sisi tulio na nguvu kuuchukua udhaifu wao wasio na nguvu, wala haitupasi kujipendeza wenye. Kila mtu mionganoni mwetu na ampendezejirani yake, apate wema, akafengwe."

Hatua ya 3      Yohana 13:35.

"Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi."

Hatua ya 7      Waefeso 4:32

"....tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu kati-ka Kristo aliyowasamehe ninyi.."

Hatua ya 11      Waefeso 4:9.

"Tendeaneni kwa ukarimu bila manung'unko."

Hatua ya 2      1 Yohana 3:16

"Katiaka hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu."

Hatua ya 6      Waefeso 4:2

"....mwenende kama inayoustahili wito wenu mlioitiwa; kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uumilivu, mkichukuliana katika upendo"

Hatua ya 10      Wagalatia 6:1.

"Ndugu zangu, mtu akighafilikatika kosa lo lote, ninyi milio wa Roho mrejezeni upya mtu kama huyo kwa roho ya upole, ukijangalia nafsi yako usije ukajarihiwa wewe mwenyewe."

Hatua ya 1      Luka 6:31.  
"Na kama mnayotaka watu wavatendee ninyi; watendeeni viyo hiyo"

"Maana ninyi, ndugu, mliitwa mpate uhuru; lakini uhuru wenu usiwe sababu ya kuufuata mwili, bali tumikaneni kwa upendo."

Hatua ya 9      Waebrahnia 3:13.  
"Lakini mwonyane kila siku, maadamu iitwapo leo; ili mmoja wenu asifanyiwe mgumu kwa udanganyifu wa dhambi"


# Cheti

Cheti hiki kimetunukiwa kwa

ambaye amekamilisha kwa kufaulu masomo yote katika kitabu hiki

## Maisha Mapya Ndani Ya Kristo Toleo la 3

Kuishi pamoja sisi kwa sisi



“Na kama mnayiotaka watu wawatende,  
ninyi watendeeni vivyo hivyo” Luka 6:31

Mwalimu

Tarehe